№230

# DAWASA YETU

WIKI HII - TOLEO NA: 230 TAREHE: 22.12.2025 HADI 28.12.2025

# WAZIRI AWESO: UPUNGUFU WA MAJI RUVU WATAMATI, DAWASA YAFIKISHENI KWA WANANCHI





Waziri wa Maji, **Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mb)** amewahakikishia wakazi wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kuwa hali ya maji katika mto Ruvu imeimarika.

Aidha, ameilekeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (**DAWASA**) kuongeza nguvu ya usambazaji na kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya uhakika.

**Mto Ruvu** ambao chanzo chake ni safu ya milima ya **Uluguru mkoani Morogoro** unachangia **asilimia 87** ya maji yote yanayozalishwa katika eneo la huduma la **DAWASA**. Mabadiliko ya tabianchi yaliathiri kiwango cha maji katika mto na kusababisha upungufu wa maji maeneo mengi ndani ya eneo la kihuduma la **DAWASA**.

**Mheshimiwa Aweso** amesema hayo wakati wa ziara katika chanzo cha mtambo wa kuzalisha maji **Ruvu Chini** kwa lengo la kukagua hali ya **Mto Ruvu** pamoja na hali ya uzalishaji.

"Hali iliyopo kama mnavyojionea inaridhisha, napenda kupongeza watendaji wote wa Bonde la **Wami Ruvu** na **DAWASA** kwa ushirikiano mzuri na ofisi za **Mikoa ya Pwani**, **Dar es Salaam** na **Morogoro** kwa kuhakikisha hali iliyotokea inapatiwa ufumbuzi," amesema.

Mheshimiwa Aweso ameilekeza **DAWASA** kuhakikisha sasa inaelekeza nguvu katika kufikisha huduma kwa wananchi baada ya huduma kuimarika.

Mbunge wa **Jimbo la Bagamoyo**, **Mheshimiwa Subira Mgalu** amepongeza sana juhudi za kurejesha mto katika hali yake ya awali na ameahidi kushirikiana na mamlaka husika katika kulinda mto dhidi ya shughuli za kijamii zinazochangia uharibifu.

"Tutakuwa bega kwa bega na **DAWASA** pamoja na bonde la **Wami Ruvu** katika kuulinda mto ili kunusuru athari zinazojitokeza kutokana na upungufu wa Maji," amesema.

Kwa upande wake, **Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA**, **Mhandisi Mkama Bwire** amesema Mamlaka inatoa uhakika wa upatikanaji wa maji na kutoa rai kwa wananchi kutoa taarifa kwa Mamlaka endapo kutatokea uharibu wa miundombinu pamoja na ukosefu wa huduma.

"Tunawashukuru wananchi kwa kuwa na sisi katika kipindi hiki, tayari maji yameongezeka hivyo sisi tunaingia mitaani kuhakikisha kila mtu anapata maji. Wananchi waendelee kututafuta kupitia **namba 181** ili kutoa tofauti," amesema.